**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU RIPOTI YAUTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA 2021 – 2022

---

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliyetujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza letu Tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mola wetu anijaalie ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili tuweze kuichangia kwa umakini wa hali ya juu na hatimae kuipitisha Ripoti iliopo mbele yetu kwa maslahi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** pia, namshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa. Hali ambayo imeendelea kuipa nafasi Serikali na wananchi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na mafanikio. Napenda kuwasisitiza viongozi pamoja na wananchi kwa ujumla tuendelee kudumisha amani na utulivu huo kwani bila ya amani hakuna maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu uwasilishwaji wa Ripoti ya Utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2021/2022 kama Kanuni ya 44(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2022 inavyoeleza.

**Mheshimiwa Spika,** nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitomshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi, na Utawala Bora

kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu ripoti ya Sita ya utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. Ripoti hii inaakisi matokeo ya kazi za msingi zilizofanywa na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma tokea ilipoanzishwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kazi nzito waliyoifanya ya kuipitia, kuijadili na kuichambua Ripoti ilioletwa mbele yao kwa upeo na ustadi wa hali ya juu. Naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii mmoja baada ya mwengine pamoja na Makatibu wao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe: Machano Othman Said | - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe: Mtumwa Peya Yussuf | - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe: Mohamed Mgaza Jecha | - | Mjumbe |
| 4. Mhe: Salma Mussa Bilali | - | Mjumbe |
| 5. Mhe: Suleiman Makame Ali | - | Mjumbe |
| 6. Mhe: Zaina Abdulla Mussa | - | Mjumbe |
| 7. Ndg: Ali Alawy Ali | - | Katibu |
| 8. Ndg: Mwanaisha Mohammed Kheir | - | Katibu |
| 9. Ndg. Amina Abeid Hemed | - | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inatoa shukurani za pekee kwa Wajumbe wawili walioalikwa kwa ajili ya kuongeza nguvu na kutoa maoni ya Ripoti hii ambao michango yao imekuwa ya kujenga na kuthaminika katika kamati yetu kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mihayo Juma N'hunga

2. Mhe. Mwanatatu Khamis Mbarak

**Mheshimiwa Spika,** aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa viongozi na watendaji wote wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kwa kazi zao nzuri na ngumu wanazozifanya katika kusimamia haki na uadilifu wa viongozi wa Umma Zanzibar, licha ya changamoto mbali mbali zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Ripoti hii ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar mbele ya Baraza lako tukufu kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,** ripoti hii kupitia tamko la mali na Madeni ya Viongozi wa Umma haijaeleza wazi sababu za msingi za kiongozi alietajwa katika jadweli kujaza fomu mara tu baada ya kiongozi huyo kumaliza mda wa kushika madaraka au wadhifa wake wa uongozi. Kamati inashauri kutolea ufafanuzi mzuri kutokana na Kamati kupata mashaka makubwa wakati wakiipitia ripoti hii huku ikijua kwamba baada ya kiongozi kama mwanasiasa kumaliza muda wake haioni sababu ya kujazishwa fomu hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia zoezi la usambazaji wa fomu za Tamko kwa viongozi mbalimbali, Kamati inashauri kuanza zoezi hilo mapema ili kuepuka kuchelewa wakati wa kuzirudisha fomu hizo. Aidha, kamati inaitaka Tume kuhakikisha agizo wanalolitoa la kujipatia fomu kupitia tovuti ya Tume ya Maadili liwe lenye kutolewa elimu endelevu kwakuwa kuna baadhi ya wajazaji wa fomu hizo hawana utaalamu wa kutosha kuhusiana na masuala ya mitandao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Tume kwa kazi ya kushajihisha zoezi la kurudisha fomu liwe katika muda uliopangwa kupitia matangazo yanatoka katika vyombo vya habari, hata hivyo ripoti hii imeonesha fomu zilizowasilishwa nje ya muda ni 11, idadi ambayo ni pungufu kulinganisha na mwaka uliopita. Kwa mnasaba huo, kamati inapendekeza kwa Tume kila inapopokea barua zinazoeleza sababu za uchelewaji wa fomu hizo, basi taarifa hizo pia zipelekwe kwenye taasisi anayotoka muhusika kwa kuwa kuchelewa kurejesha fomu kwa wakati na bila ya sababu za msingi ni kosa la kimaadili.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia ripoti hii, Tume imeeleza kufanyika uhakiki wa taarifa za mali na madeni ya viongozi wa Umma kwa lengo la kuhakikisha usahihi wa taarifa hizo. Kamati inapata wasiwasi juu ya vigezo na sifa zinazotumika katika uhakiki huo kwa kuwa imeonekana kuwa viongozi

wachache sana wanaohakikiwa na kuonekana kuna upungufu wa nyaraka za umiliki wa mali hizo ambazo zinahakikiwa kila mwaka. Kamati inaishauri Tume kuandaa utaratibu maalumu wa kuwawezesha viongozi hao kufanyiwa uhakiki kila inapohitajika lakini pia kuwatafutia njia mbadala za kuwasaidia katika uhaulishaji wa mali hizo kwa urahisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaipongeza Tume katika suala zima la uimarishaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa usajili wa Taarifa za Mali na Madeni pamoja na kutunza taarifa za uhakiki wa mali za viongozi, kwa kuwa suala hilo litarahisisha ufanyaji kazi kwa njia iliyo bora zaidi. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwepo kwa usiri mkubwa katika utunzaji na uhifadhi wa taarifa hizo kwa ujumla, sambamba na kuwepo kwa hatua za kisheria na kinidhamu kwa yeyote ataevuka miko ya uvujishaji wa taarifa hizo.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, katika kupokea na kuchunguza tuhuma na malalamiko ya ukiukwaji wa sheria na maadili ya viongozi wa umma Kamati inaitaka Tume kutoa ufafanuzi wa malalamiko yaliyojikita katika upande wa udhalilishaji wa kijinsia ambalo moja ya lalamiko upelelezi wake umekamilika na muhusika anasubiri kuitwa mbele ya Tume kujibu tuhuma hizo badala ya tuhuma hizo kuzifikisha katika Mahkama kisheria. Aidha, Kamati inataka kufahamu zaidi kuhusu kesi hizi ambazo msingi wake ni makosa ya jinai, je muhusika baada ya kukutwa na hatia, hatua inayofuata kwa upanda wa Tume ni ipi, kutumia Sheria ya Tume ya Maadili au kwenda na utaratibu wa kutumia Sheria Nam. 7 ya Mwaka 2018 ambayo inasimamia kesi za jinai.


**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Tume kwa hatua za mafunzo ya kitaalamu kwa wafanyakazi wake. hata hivyo, Kamati inatoa msisitizo kwa Tume kutekeleza mafunzo ambayo yanalenga zaidi na majukumu ya Tume ya Maadili ili yaweze kuleta tija kwa wafanyakazi hao na kurahisisha kazi zao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaridhika sana na kazi nzuri za Tume ya Maadili ya

Viongozi wa Umma Zanzibar ya kuhakikisha kwamba inasimamia maadili ya viongozi na imepata mafanikio kwa mujibu utekelezaji wa kazi zao wanazojipangia kuzitekeleza kila mwaka. Aidha, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Tume ya Maadili kwa kuwa ni taasisi ya mfano katika kuwasilisha ripoti yake Barazani kwa wakati. Nachukua nafasi hii kuziomba taasisi nyengine ambazo zinatakiwa kuwasilisha ripoti hizo kufanya hivyo kwa wakati unaofaa.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii, na pia nazidi kuwashukuru wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano yao makubwa waliyonipatia pamoja na kuwa na msimamo na umakini kwa wanachokisimamia.

**Mheshimiwa Spika: Naomba Kuwasilisha.**



……………………………………

**(*Machano Othman Said*)**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa**

**Baraza la Wawakilishi,**

**<u>Zanzibar</u>**